


Viini Saba vya

Mafundisho Jamii ya Kikatoliki kwa watoto




1 UHAI WA MTU NA HESHIMA YA MTU

Mungu aliumba kila mtu, hivyo uhai wa kila mtu ni muhimu sana na ni lazima ulindwe.




2 WITO KWA FAMILIA, JUMUIA NA KUSHIRIKI

Mungu alituumba na tuwe sehemu ya jamii, familia na Nchi, watu wote waweze kushirikiana na kusaidiana.




3 HAKI NA MAJUKUMU

Mungu angependa sisi sote tusaidie kuhakikisha uwepo wa usalama na afya ya kila mmoja wetu ili sote tuwe na maisha mazuri.




4 CHAGUO KWA AJILI YA MASKINI NA WASIOJIWEZA

Mungu angependa sisi sote tuwasaidie wenzetu walio maskini, wasiokuwa na chakula cha kutosha, mahala salama pa kuishi wala jumua.




5 HESHIMA KWA KAZI NA HAKI ZA WAFANYAKAZI

Jinsi Mungu alivyopanga, kazi ni muhimu kwa watu wazi ma na kwa familia zao, hivyo haki inapaswa kutendwa katika kuwaajiri watu na katika malipo ya ajira zao.



6 MSHIKAMANO

Mungu aliumba kila mmoja wetu, kwa hivyo, popote pale tuishipo, sisi sote ni ndugu na dada katika familia ya Mungu.



7 KULINDA VIUMBE VYA MUNGU

Ulimwengu uliumbwa na Mungu hivyo tunapaswa kutunza viumbe vyote.



Mada hizi zimezalishwa na Muungano wa Maaskofu wa Kanisa Katoliki la Marekani, *Kushiriki Mafundisho Jamii ya Kikatoliki: Changamoto na Maelekezo* Hati miliki 2017 Muungano wa Maaskofu wa Kanisa Katoliki la Marekani na Huduma za Misaada za Kanisa Katoliki.

Haki zote zimehifadhiwa. Picha kwa heshima ya Ndugu Mickey McGrath, OSFS.